SHULE YA SEKONDARI YA MT. AUGUSTINO
(ST. AUGUSTINE SECONDARY SCHOOL)

S. L. P. 31644, DAR ES SALAAM

SHERIA ZA SHULE

Kama ilivyotajwa hapo awali, kuwa shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu (The Education Act Chapter 353 RE 2002) na marekebisho yake yote. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu hapa Tanzania. Kwa ajili ya ufanisi, unatakiwa kuzingatia sheria na kanuni hizi kwa kipindi chote utakachokuwa hapa shuleni.

1. **KUMWABUDU MUNGU:** Wanafunzi WOTE watamwabudu Mungu kadiri ya Utaratibu wa Kanisa Katoliki.

2. Akiwa hapa shuleni mwanafunzi atatakiwa kufikisha wastani wa 51 (C) katika kidato cha I na II na wastani wa 61 (B) katika kidato cha III na IV kila muhula. Kushindwa kufikisha wastani huo kutamwondolea mwanafunzi sifa ya kuendelea na masomo katika Sekondari yetu.

3. Mwanafunzi anatakiwa kuonesha bidii na akiwa shuleni atashiriki shughuli zote watakazoshiriki wenzake kama vile kusali na kufanya usafi wa mazingira na shughuli zingine zitakazoelekezwa na uongozi wa shule.

4. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa mtii, kujiheshimu yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine: walimu, wafanyakazi, viranja pamoja na wanafunzi wenzake.

5. Ni muhimu na wajibu kwa kila mwanafunzi kuwahi mahali popote atakapohitajika: darasani, mihadharani, michezoni na kazini.

6. Ni marufuku kwenda nje ya eneo la shule bila ruhusa ya uongozi unaohusika.

7. Mgeni yeyote lazima atambulishwe kwa Mwalimu wa Zamu kabla ya kukaribishwa kumwona mwanafunzi.

8. Siku ya Wazazi kuwaona watoto wao itakuwa kila Jumapili ya mwisho wa mwezi. Ni marufuku kwa mzazi yeyote kumletea mtoto wake chakula cha aina yoyote (na vitu vingine vilivyotajwa katika na. 22 na 25) kwani kitendo hicho kitaambatana na kumchukua mtoto kurudi naye nyumbani.

9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana ndani au kwenye mazingira ya nyumba za kulala wageni/hoteli.

10. Kila mwanafunzi ni lazima atunze ukimya muda wote awapo darasani, maktabani, na mahali popote atakapotakiwa kufanya hivyo.

11. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza siha na usafi wake binafsi na wa mazingira yote ya shule.

12. Kila mwanafunzi atawajibika kulinda na kutunza mali ya shule na yake binafsi. Mwanafunzi atakayeharibu mali ya shule atapaswa kulipa mara moja baada ya kuthibitika.

13. Lugha ya mawasiliano mwanafunzi awapo shuleni ni Kiingereza. Kiswahili kitatumika katika vipindi vya somo hilo darasani, wakati wa kujadiliana somo hili katika vikundi vya kujisomea, Kanisani, na matukio maalum kama itaamriwa hivyo na uongozi husika. Mwanafunzi yeyote atakayebainika kutumia Kiswahili nje ya muda uliotajwa hapo juu au kutumia lugha nyingine yoyote ile, ataadhibiwa.

14. Kubaki nyumbani kwa sababu ya ugonjwa hakutakuwa na msamaha wowote endapo mwanafunzi hakupewa ruhusa kimaandishi. Mwanafunzi asiyefika shuleni pasipo ruhusa atahesabiwa kuwa mtoro tendo ambalo baadaye linaweza kusababisha kuondolewa shuleni.

15. Ugomvi au kupigana, kuleta fujo darasani au eneo lolote la shule, lugha chafu na matusi, kashfa kwa wenzako au raia ni mwiko kabisa. Shuleni ni mahali pa kuheshimiana, vitendo vya unyanyasaji wa madarasa ya chini na wageni havitavumiliwa.

16. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutumia vitu ambavyo vitamwingizia gharama isiyokuwa na umuhimu kama vile matumizi ya vipodozi, kusuka nywele, kupaka wanja, kupaka rangi kucha, na mitindo mbalimbali ya wanaume ya kunyoa nywele. Kwa wasichana ni marufuku kusuka nywele.

17. Wizi ni kosa kubwa sana. Adhabu yake ni kufukuzwa shule.

18. Vitendo vyovyote vya kushiriki au kushawishi mgomo wa aina yoyote shuleni adhabu yake ni kufukuzwa shule.

19. Pamoja na kosa la wizi na kushawishi mgomo ambayo adhabu yake ni kufukuzwa, makosa mengine yenye adhabu ya kufukuzwa ni pamoja na: uasherati, ulevi, ubakaji na ushoga, kudharau bendera ya Taifa, kuoa na kuolewa, kuharibu kwa makusudi mali za umma, kuvuruga amani na usalama shuleni, kukataa adhabu halali, utoro, kutoroka mitihani na mazoezi, kupata mimba, uvutaji sigara/bangi/mirungi, madawa ya kulevya, dawa za uzazi wa mpango, n.k.

20. Siku zote awapo shuleni mwanafunzi atakula chakula kitakachopatikana ndani ya eneo la shule tu na kitaliwa kantini si mahali pengine.

21. Kila mwanafunzi ni lazima avae sare ya shule muda wote awapo ndani ya eneo la shule isipokuwa kwa kesi maalum itakayothibitishwa na uongozi.

22. Nyumba za watumishi ni nje ya eneo la shule. Ruhusa maalum itafutwe kutoka kwa Mwalimu wa Zamu au Mshauri wa Wanafunzi (Patron/Matron) kama kuna umuhimu wa mwanafunzi kufika huko muda wa shule au muda mwingine wowote.

23. Redio, simu za mkononi, na vifaa vyovyote vya umeme haviruhusiwi kabisa shuleni. Pia hairuhusiwi kuunganisha au kung'oa *sockets, switch* au *bulb-holders* au nyaya za umeme popote pale katika majengo ya shule au sehemu za kulala.

24. **Adhabu:** Mwanafunzi akivunja mojawapo ya kanuni za mwenendo bora anaweza kupewa adhabu na Kiongozi wake (mwanafunzi) au Mwalimu kutegemea uzito wa kosa.

25. **Dini:** Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujishughulisha na kuhubiri itikadi za dini awapo shuleni, wala kuudai uongozi utimize taratibu na sera za dini au dhehebu lake.

26. **Fedha za mkononi:** Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kukaa na fedha. Fedha zote zitakabidhiwa kwa Mhasibu wa Shule na zitatumika kwa ridhaa ya mwanafunzi mwenyewe kimaandishi au mzazi ikiwa ni jambo muhimu.

27. **Malipo:** Malipo yote yatafanyika benki. Shule haitampokea wala kushughulikia kesi ya mwanafunzi yeyote itakayosababishwa na huduma ya benki kama vile upokeaji wa risiti feki.

MUHIMU:
Kwa makosa yale yanayovumilika mwanafunzi atapata onyo kimaandishi mara tatu na mara ya nne onyo litaambatanishwa na barua ya kufukuzwa shule.

Wako katika Utumishi,

……..
Padre Erastus Elias Mgani, OSA
Mkuu wa Shule